

# Kileo—Wewe Utafanya Nini?



# 1

Upo kwenye tafrija na unatambua kwamba baadhi ya vijana wanakunywa kileo ingawa hawaruhusiwi kufanya hivyo.

## Utafanya nini?

### TULIA NA UFIKIRI!

BIBLIA INASEMA HIVI: “Mtu mwerevu ni yule ambaye ameona msiba na kujificha, lakini wasio na uzoefu wameendelea mbele nao lazima waumie.”—Methali 22:3.

### Ukiwa na wazo hilo akilini, jibu maswali yafuatayo.

Ni jambo gani linaloweza kutokea ukiendelea kukaa kwenye tafrija hiyo?

---



---

Unawezaje kuondoka hapo bila kuanzisha mzozo au kudhihakiwa?

---



---



---

Je, dhihaka ndilo jambo *baya zaidi* linaloweza kutokea?

---



---



## DOKEZO

Fanya mpango mapema na wazazi wako ili uwapigie simu au kuwaandikia ujumbe wa simu ukihitaji kuondoka haraka katika tafrija hiyo.

Nitafanya nini ikiwa nipo kwenye tafrija ambayo watu wanakunywa kileo kupita kiasi:

---



---



---



---



2

Mtu fulani anajaribu kukulazimisha unywe kileo. Utafanya nini?

**TULIA NA UFIKIRI!**

BIBLIA INASEMA HIVI: “Ninyi ni watumwa wake kwa sababu mnamtii yeye.” —Waroma 6:16.



**Ukiwa na wazo hilo akilini, jibu maswali yafuatayo.**

Nini kinachoweza kutokea ikiwa hutatoa jibu kwa uthabiti?

---



---

Kujiamini kunaweza kukusaidiaje kukataa ushawishi wa vijana wenzako?

---



---



---

**DOKEZO**

Tayarisha mapema jambo la kusema. “Kwa kawaida mimi husema, ‘Hapana, siko tayari sasa.’ Hilo hufanya watu waache kunisumbua na kwa kawaida hawajaribu tena kunilazimisha.” —Brianna

Nitasema nini ikiwa mtu fulani anajaribu kunilazimisha ninywe kileo:

---



---



---

# 3

Unaenda matembezi pamoja na marafiki na unatambua kwamba dereva wa gari lenu ameleva.

## Utafanya nini?



### TULIA NA UFIKIRI!

BIBLIA INASEMA HIVI: “Anayetembea na watu wenye hekima atakuwa na hekima, lakini anayeshirikiana na wajinga atapatwa na mabaya.”  
—Methali 13:20.

### Ukiwa na wazo hilo akilini, jibu maswali yafuatayo.

Ni jambo gani linaloweza kutokea ikiwa utamruhusu mtu huyo aendeshe gari kurudi nyumbani?

---

---

Unaweza kufanya uamuzi gani?

---

---

---

Matendo yako yanaweza kumsaidiaje dereva huyo na wengine?

---

---



## DOKEZO

Epuka hali zitakazofanya uendeshwe na dereva ambaye sifa zake zinatiliwa shaka. Sikuzote uwe na mpango wa badala wa usafiri.

Nitafanya hivi ikiwa dereva anayeendesha gari ameleva:

---

---

---